# HABARI na MATUKIO

Toleo Na. 30 | Tanzania Fertilizer Regulatory Authority | tfra_official | tfra_official | Septemba 2025

JARIDA LA KILA MWEZI LA MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA


## WILAYA YA KIGOMA YAMPONGEZA RAIS SAMIA KWA KUTOA RUZUKU YA MBOLEA



Wajumbe wa bodi na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) wakiwa katika picha ya Pamoja na Mkuu wa wilaya ya Kasulu, Kanali Isaack Anthony (Katikati) wakati wa ziara ya bodi wilayani humo tarehe 9 Septemba, 2025, mkoani Kigoma.


NDANI>>

TFRA Yawahakikishia wakulima wa Songwe upatikanaji wa mbolea pindi msimu utakapoanza 4

Wakulima wahakikishiwa upatikanaji mbolea za kutosha msimu ujao 2025/2026 5

# Wilaya ya Kigoma yampongeza Rais Samia kwa kutoa Ruzuku ya Mbolea



Mhandisi Amon Ntemba ambaye ni Mmiliki wa Kibondo Green Farm akiwaaelezea Wajumbe wa Bodi na Menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) jinsi mbolea inavyoongeza tija katika uzalishaji hususan kwenye zao la parachichi tarehe 9 Septemba 2025.

Rais Samia Suluhu Hassan amepongezwa kwa kutoa Ruzuku ya Mbolea iliyochangia matumizi yake na kuchochea uzalishaji wa mazao mbalimbali ya kilimo nchini.

Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, Kanali Isaack Anthony, alitoa pongezi hizo alipokuwa akizungumza na Wajumbe wa Bodi na Menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) waliopo mkoani Kigoma kwa ziara iliyolenga kuhamasisha upimaji wa afya ya udongo na matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima wa mkoa huo.

Alisema wananchi wengi wa wilaya yake ni wakulima, na mpango huo wa ruzuku umewasaidia kwa kiasi kikubwa kupata mbolea kwa bei nafuu na kuongeza mavuno.

Naye mmiliki wa shamba la parachichi, Mhandisi Amon Daniel Ntimba, aliipongeza serikali kwa kuja na mpango wa ruzuku ulioleta mapinduzi katika kilimo na kuahidi kuongeza matumizi ya mbolea kutokana na wakulima wengi kumudu bei ya pembejeo hiyo tofauti na ilivyokuwa kabla ya kuanzishwa mpango wa ruzuku.

Alisema wakulima wengi wameongeza uzalishaji na uchumi wao umekua kwa kuzalisha mazao mengi ya chakula na kuyauza ili kumudu mahitaji mengine.

Akizungumza katika ziara hiyo, Mjumbe wa Bodi ya TFRA, Khadija Jabri, aliwahimiza wakulima na wawekezaji kupima sampuli za udongo ili kuhakikisha wanatumia mbolea sahihi kulingana na mahitaji ya udongo na zao linalolimwa.

Katika ziara hiyo, wajumbe wa bodi walitembelea Kiwanda cha Sukari Kasulu na shamba la parachichi la Kibondo Green Farm lililopo wilayani Kibondo mkoani Kigoma.



Mkuu wa wilaya ya Kasulu, akitoa pongezi kwa Wajumbe wa Bodi na Menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA) kwa kuhakikisha mbolea za ruzuku zinapatikana katika wilaya yake ambayo ina wakulima wengi wanaotumia mbolea kuongeza tija ya uzalishaji.

# Wilaya ya Kigoma yampongeza Rais Samia kwa kutoa Ruzuku ya Mbolea



Mjumbe wa bodi TFRA Hadija Jabir (kushoto) pamoja na Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi Victoria Elangwa (kulia) wakiwa na Mkurugenzi mtendaji wa NDF Amos Byejwe (katikati) katika vitalu vya miche ya michikichi Mlole, Kigoma tarehe 9 Sepetemba 2025.



Mkurugenzi Mtendaji wa NDF, Amos Aron Byejwe akiwaonyesha wajumbe wa bodi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) namna matumizi sahihi mbolea yanavoongeza uzalishaji wa miche ya michikichi Mlole, Kigoma tarehe 9 Septemba 2025.



Mkurugenzi Mtendaji wa Ndugu Development Foundation (NDF), Amos Aron Byejwe, akieleza namna anavyozalisha mbegu bora za miche ya michikichi kwa kutumia mbolea, hususan zile zinazotolewa kwa ruzuku, wakati wa ziara ya Bodi ya TFRA tarehe 9 Septemba 2025.

# TFRA Yawahakikishia wakulima wa Songwe upatikanaji wa mbolea pindi msimu utakapoanza



Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Jabir Makame (katikati), akizungumza kwenye kikao na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent kikao hicho kililenga kujadili na kuhakikisha upatikanaji wa mbolea kuelekea msimu wa kilimo kikao hiko kilifanyika tarehe 25 Septemba, 2025 mkoani humo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent, amewahakikishia wakulima wa mkoa wa Songwe upatikanaji wa mbolea kwa msimu ujao wa kilimo.

Akizungumza leo tarehe 25 Septemba 2025 katika kikao na Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Jabiri Makame, kilichofanyika katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Laurent amesema ziara yake mkoani humo inalengo la kusalimia, kujitambulisha na kutoa taarifa ya hali ya upatikanaji wa mbolea mkoani humo.

Kwa upande wake Mhe. Makame ameahidi ushirikiano wa kutosha kutoka Serikali ya Mkoa wa Songwe katika kuhakikisha tasnia ya mbolea inasimamiwa ipasavyo.

Aidha, amebainisha umuhimu wa Mkoa huo kwa Taifa ikiwa ni mkoa wa pili kwenye matumizi makubwa ya mbolea na ni miongoni mwa mikoa mitano inayoongoza



Wadau wa mbalimbali wa kilimo wakiwa katika kikao cha kujadili mikakati ya kuhakikisha upatikanaji wa mbolea kuelekea msimu wa kilimo kilichofanyika tarehe 25 Septemba, 2025 kilichofanyika katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe.

# Wakulima wahakikishiwa upatikanaji mbolea za kutosha msimu ujao 2025/2026

Kuelekea msimu mpya wa kilimo wa 2025/2026,. waingizaji na wazalishaji wa mbolea nchini wamewahakikishia wakulima kuwa mbolea za kupandia na kukuzia zitapatikana kwa wingi na kwa wakati.

Kutokana na uhakika huo, wakulima wametakiwa kujipanga mapema na kuanza kununua mbolea hizo kabla ya msimu kuanza rasmi.

Uhakika huo ulijulikana kufuatia ziara ya ukaguzi iliyofanywa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Bw. Joel Laurent, pamoja na watendaji wengine wa Mamlaka hiyo, walipotembelea maghala na vituo vya usambazaji vya waingizaji wa mbolea nchini.

TFRA imehakiki KUuwepo kwa tani 52,316.10 za mbolea za kupandia na tani 159,800.66 za mbolea za kukuzia, huku tani 86,052 za mbolea za kupandia na tani 74,261 za mbolea za kukuzia zikiwa zinatarajiwa kuwasili nchini mwanzoni mwa Oktoba 2025.

Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya uingizaji wa Mbolea ya Premium, Brijesh Barot, alisema kampuni yake imeongeza uingizaji kutoka tani 80,000 hadi kufikia tani 100,000, huku Mkurugenzi Mtendaji wa DRTC Fertilizers, Bernad Kajamiti, akibainisha kuwa wameongeza mbolea za kupandia kutoka tani 10,000 hadi tani 15,000 msimu huu.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa YARA Tanzania, Winstone Odhiambo, alisema kufikia Oktoba 2025 kampuni yake itakuwa na zaidi ya tani 37,000 za mbolea za kupandia zitakazosambazwa nchini kote.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Samuel Mshote, alisema kampuni yake ina tani 8,661 cha mbolea za kupandia na tani 11,173 cha mbolea za kukuzia kwa sasa huku wakitarajia kuingiza tani 20,000 cha mbolea za kupandia mwanzoni mwa Oktoba.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya mbolea ya ETG Input, Ranjeet Kumar, akiwasilisha taarifa ya kiasi cha mbolea kilichopo nchini, alisema kampuni yake ina jumla ya tani 17,525.14 cha mbolea za kupandia na tani 86,639.70 cha mbolea za kukuzia huku wakitarajia kupokea shehena ya tani 15,000 za mbolea za kupandia na tani 50,000 za mbolea za kukuzia.

Meneja Mkazi wa kampuni ya OCP Tanzania, Hilary Pato, aliieleza Mamlaka katika kikao kilichofanyika kwa njia ya mtandao baada ya uongozi wa juu wa TFRA kutembelea maghala ya kampuni hiyo kuwa kampuni yake ina tani 13,676.87 za mbolea za kupandia na tani 920.33 za mbolea za kukuzia huku tani 35,000 zikitarajiwa kuwasili nchini wakati wowote kuwawezesha wakulima kupata bidhaa hiyo kwa wakati.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa MET Fertilizer, Indrabhuwan Singh, alisema kampuni yake imejipanga kuhakikisha wakulima wanapata mbolea za kukuzia kwa wingi ili kuongeza tija kwenye uzalishaji huku akibainisha kuwa mpaka sasa kuna tani 60,000 za mbolea za kukuzia na kuzalishia katika maghala yao tayari kuwahudumia wakulima.

Waingizaji hao wamekiri ongezeko hilo la uagizaji wa mbolea limechochewa na ruzuku ya mbolea inayotolewa na serikali pamoja na elimu endelevu ya matumizi sahihi ya pembejeo hiyo.

Naye Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea Kwa Pamoja wa TFRA, Loius Kasera, alisisiitiza kuwa ni wajibu wa Mamlaka kuhakikisha kuwa mbolea inapatikana kwa bei nafuu na kwa wakati.

Aliwataka wakulima kote nchini kuanza kununua mbolea mapema kabla ya kuanza kwa msimu ili kuepuka usumbufu, huku akiwataka waingizaji kuendelea kuongeza shehena ili bidhaa hiyo isikosekane sokoni.

“Tunawaomba wakulima waendelee kujitokeza mapema kununua mbolea kwa kuwa ipo ya kutosha. Tunalinda maslahi yenu na tija ya kilimo,” alisema. Kasera.

Kampuni za uingizaji wa mbolea zilizotembelewa ni pamoja na ETG Inputs Limited, Yara Tanzania, STACO Agrochem Limited, OCP Tanzania Limited, Tanzania Fertilizer Company na DRTC Limited.



Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, akipokea maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya mbolea ya ETG Input, Ranjeet Kumar, alipofanya ziara katika ghala la kampuni hiyo kujihakikishia upatikanaji wa mbolea kwa wingi katika msimu huu mpya wa kilimo.

# Wakulima wahakikishiwa upatikanaji mbolea za kutosha msimu ujao 2025/2026




Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, akiwa katika picha ya pamoja na wafanyakazi wa Kampuni ya ETG baada ya kutembelea na kujionea shughuli mbalimbali za kampuni hiyo.



Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, akisaini kitabu cha wageni cha Kampuni ya mbolea ya STACO Agrochem Limited wakati wa ziara ya kuhakikisha upatikanaji wa mbolea za kutosha kuelekea msimu wa kilimo wa 2025/2026.



Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, akiwa pamoja na Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea, Louis Kasera, na Meneja wa Uingizaji na Usafirishaji wa Mbolea, Dotto Diteba, wakiwa katika ghala la mbolea la Kampuni ya MO Fertilizer wakati wa ziara iliyofanywa na Mamlaka ili kuhakikisha kuwa mbolea zinapatikana kwa wingi nchini kuelekea msimu wa kilimo wa 2025/2026.



Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, akiwa pamoja na Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea, Louis Kasera, na Meneja wa Uingizaji na Usafirishaji wa Mbolea, Dotto Diteba, wakiwa kwenye kikao na wafanyabiashara wa mbolea kutoka Kampuni ya ETG Inputs Limited.

# Wakulima wahakikishiwa upatikanaji mbolea za kutosha msimu ujao 2025/2026



Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, akiwa pamoja na Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea, Louis Kasera, Meneja wa Uingizaji na Usafirishaji wa Mbolea, Dotto Diteba, na Meneja Kanda ya Mashariki, Daniel Maarifa, wakiwa katika ghala la mbolea la Kampuni ya STACO Agrochem Limited wakati wa ziara iliyofanywa na Mamlaka hiyo kuhakikisha upatikanaji wa mbolea za kutosha nchini kuelekea msimu wa kilimo wa 2025/2026.



Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, joel Laurent, akiwa na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Uingizaji wa Mbolea ya Premium, Brijesh Barot, katika sehemu ya mitambo ya kufunga mbolea



Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Uingizaji wa Mbolea ya Premium, Brijesh Barot, akimwonyesha Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA,, Joel Laurent, mashine ya kufunga mbolea iliyopo kiwandani kwao.



Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, akiwa pamoja na Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea, Louis Kasera, na Mkurugenzi Mkuu wa Tanzania Fertilizer Company, wakiwa kwenye ziara iliyofanywa na Mamlaka ili kuhakikisha upatikanaji wa mbolea wa kutosha nchini kuelekea msimu wa kilimo wa 2025/2026.

# TFRA, ujumbe wa Oman washiriki mkutano wa kibiashara Dar



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Elizabeth Bolle, pamoja na Kaimu Mkurugenzi wa Uzalisishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja, Getrude Ng'weshemi, wakiwa pamoja na watumishi wengine wa TFRA wakifuatilia mkutano wa Wafanyabiashara kutoka Oman, uliofanyika tarehe 8 katika Hoteli ya Johari Rotana, jijini Dar es Salaam.

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) ilipata fursa ya kushiriki mkutano mkutano wa kibiashara na ujumbe ujumbe wa wafanyabiashara kutoka Oman, mkutano ambao ulifanyika jijini Dar es Salaam.

Mkutano huo uliandaliwa kwa lengo la kujadili fursa mbalimbali za uwekezaji baina ya Tanzania na Oman, hususan katika nyanja za kilimo, viwanda na biashara, sambamba na kumarisha upatikanaji wa bidhaa kati ya matalfa hayo mawili.

Kupitia majadiliano, pande zote mbili zilikubaliana kuongeza ushirikiano wa kibiashara na kiuwekezaji, huku Tanzania ikiwahakikishia wawekezaji hao mazingira wezeshi, salama, rafiki na yenye fursa pana za uwekezaji.

Ujumbe wa Oman ulionesha utayari kushirikiana na Tanzania katika kuendeleza miradi ya biashara na uwekezaji yenye manufaa kwa pande zote mbili.

Pamoja na makubaliano hayo, Tanzania na Oman ziliahidi kuendeleza majadiliano zaidi ili kuwezesha utekelezaji wa mikakati ya pamoja ya kukuza biashara na uwekezaji

Mkutano huo ulihudhuriwa na Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Hashil Abdallah, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Dkt. Stephen Nindi, Wakuu wa Taasisi na wadau mbalimbali kutoka Sekta za Kilimo, Viwanda na Biashara pamoja na mashirika binafsi.

TFRA, iliwakilishwa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Elizabeth Bolle, Kaimu Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja, Getrude Ng'weshemi, na watumishi wengine walioambatana nao.

# Madini ya viwandani kuchochea uwekezaji viwanda vya mbolea nchini



Mkurugenzi wa Tanga Mining Limited, Bw. Rishit Lalseta, alisema madini ya viwandani hususan dolomite yamekuwa na mchango mkubwa katika kuendeleza viwanda vya mbolea na hatimaye kuchochea ukuaji wa sekta ya kilimo nchini.

Amesema hayo alipokuwa akizungumza na Madini Diary tarehe 10 Septemba, 2025 jijini Tanga, ambapo alisema kuwa dolomite ni nyenzo muhimu sana kwenye utengenezaji wa mbolea kwa sababu huongezakalsiamu na magnesiamu kwenye udongo, kurekebisha asidi na hivyo kufanya mazao kukua kwa afya na kutoa mavuno bora.

"Kwa maana hiyo, sekta ya kilimo inapewa nguvu ya ziada na wakulima kunufaika zaidi kupitia matumizi ya mbolea zenye virutubisho vinavyotokana na madinihaya," alisema Lalseta.



Ameongeza kuwa hatua hii ni kielelezo cha namna sekta ya madini inavyoweza kuunganisha sekta nyinginemuhimu nchini ikiwemo viwanda, kilimo na ujenzi, jambolinalosaidia kufanikisha ajenda ya taifa ya uchumi wa viwanda na maendeleo endelevu.

Aidha, alibainisha kuwa kiwanda cha Tanga Mining Limited kilichoanzishwa mwaka 2014 kimekuwa chanzo cha ajira kwa wananchi wa Tanga na maeneo jirani, sambamba na kuchangia mapato ya Serikali kupitia kodi na tozo mbalimbali.

Kwa mujibu wa Lalseta, soko la mbolea nchini bado ni kubwa na mahitaji ni makubwa, hivyo kwa sasa kampuni inajikita zaidi katika soko la ndani lakini pia inalenga kupanua wigo na kuingia kwenye masoko ya kimataifa ilikuisaidia nchi kuongeza fedha za kigeni kupitia bidhaa zinazozalishwa ndani.

# Ujumbe wa TFRA watembelea kiwanda cha mbolea Bahi

Ujumbe wa Mamlaka ya TFRA kutoka Sehemu ya Uhamasishaji, Uzalishaji wa Ndani na Mazingira, ikiongozwa na Meneja wa Kanda ya Kati, Allan Mariki, ulitembelea kiwanda kipya cha ALMAH AGRO GROUP LIMITED kilichopo Mpamatwa, Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma Septemba 23, 2025 kuangalia upatikanaji wa mbolea nchini kuelekea msimu wa kilimo wa 2025/2026.

Kiwanda hiki kinazalisha mbolea ya maji iitwayo Agri Gold Super Booster, na pia kipo kwenye maandalizi ya kuzalisha mbolea ngumu (granules) kwa kutumia malighafi ya samadi.

Uzalishaji wa mbolea ngumu unatarajiwa kuanza Oktoba 2025 ambapo kiwanda kimepanga kuzalisha hadi tani 30 kwa siku.

Mitambo ya kisasa inaendelea kusimikwa ili kuhakikisha uzalishaji unafanyika kwa ufanisi.

Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Halima Babu Karim, alisema kuwa kampuni yake imekusudia kuzalisha mbolea bora na tayari imeandaa wataalam pamoja na wafanyakazi watakaopatiwa mafunzo ya teknolojia kusimamia uzalishaji.

Kampuni imekusanya zaidi ya tani 42,000 za samadi kama malighafi ya mbolea ngumu (granules) na pia imeanzisha mashamba darasa kwa ajili ya majaribio ya mbolea yao ya maji, ambayo yameonesha mafanikio makubwa kwenye mazao mbalimbali.

Hatua hii inalenga kuwajengea wakulima imani kuhusu ubora wa mbolea na kuongeza kasi ya matumizi mara baada ya kuingia sokoni.

Timu ya TFRA iliipongeza kampuni na kuwatia moyo viongozi wake kwa hatua kubwa waliyoifikia, ikizingatiwa kwamba uwekezaji huu una dhamira ya dhati ya kuhudumia wakulima kwa kuhakikisha upatikanaji wa mbolea bora nchini, jambo ambalo ni muhimu katika kuongeza tija ya kilimo.

Mamlaka ilimhakikishia Mkurugenzi wa kampuni pamoja na timu yake ushirikiano wa karibu katika kukamilisha taratibu zinazohitajika, huku TFRA ikiamini uwepo wa kiwanda hiki utachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza upatikanaji wa mbolea bora kwa wakulima na kuchochea maendeleo ya kilimo nchini.




Mkurugenzi wa kiwanda cha Agri Gold Super Booster, Halima Babu Karim katikati akiwa na Meneja sehemu ya Uzalishaji wa Ndani wa Mbolea na Mazingira wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Getrude Angel Ng'wesheni wa pili kushoto na watalaam kutoka TFRA walipotembea kiwanda hicho jijini Dodoma tarehe 23 Septemba 2025.